Kurudi

na

J. D. Logan

Kurudi

na

J. D. Logan

Octoba 11, 2011

Kurudi

Mtu leo anasikia sana kuhusu "kuadhimu" au kurudi kwa Israeli kama jinsi ilivyonenwa na manabii. Tunafanywa kuamini na "wasomi wengi wa biblia" kwamba kutakuwa na mkutano wa jumla wa Waebrania katika mataifa yote. Wengine hata wanashuhudia kwamba dunia yote itazingirwa na watu wa Mungu, wakihusika na "mkusanyiko" wa Wayahudi.

Je ndivyo inavyofundishwa katika maandiko? Kama kweli hili ndilo shauri la kila mtu, inatusukuma sote kujifunza neno la Mungu ili kuelewa ni nini yaliyo makusudi yake kwetu.

Baraka za Mungu … Laana

Musa alimhakikishia Israeli kwamba "*…Mungu atakuweka juu ya mataifa yote ya dunia*". (Kumb.28:1-14) Kusingekuwa na baraka yo yote ambayo ingezuiwa kama wangetunza amri za Mungu.

Kwa upande mwingine, kama wakimkataa Mungu na amri zake, Mungu angezidisha laana yake kwa Waisraeli wote. (Kumb.28:15-28)

Israeli, kupitia historia yake kama watu wa Mungu aliowachagua, waliendelea kuhasi amri za Mungu na wazinzi wakaendelea kuabudu miungu, wakitafuta kuishi kama mataifa mengine ambao hawakumjua Mungu.

Kwa sababu ya hili, Mungu mara zote aliendelea kusababisha laana yake juu yao katika mtindo wa kuvamiwa na majeshi, ikisababisha uhamisho wao katika mataifa mengine; "*…utapigwa mbele za maadui zako…na utaondolewa kutoka katika falme zote za dunia.*" (Kumb 28:25).

Wa kwanza kutawanyika … Israeli

Ikifuatiwa na mgawanyiko wa ufalme wa Wayunani, ikifuatiwa na kifo cha Sulemani, sehemu ya kaskazini (iliyojulikana kama Israeli… wakagawanyika kutoka Yuda), wafalme wa Waisraeli na watu wakawa dhaifu na wabudu sanamu ambao Mungu alileta katika Ashuru na kuwatoa katika nchi. Hivi ndivyo ilivyokuwa sehemu pana ya Wayunani. "*Basi Bwana alichukizwa na Israeli na kuwatoa mbele ya macho yake: hakuna aliyebaki isipokuwa kabila la Yuda pekee.*" (2 Wafalme 17:17-18).

Wengine wanachukulia kuondolewa huku kama "makabila kumi yaliyopotea" na kujaribu kusisitiza "kuzunguka kwao" katika Uropa yote. Haya ni mitazamo ya wazi yaliyojaa na mafundisho ya uongo na hayatowi ushahidi kutoka na ukweli uliotolewa katika maandiko.

Wa pili kutawanyika … Yuda

Yuda walichukuliwa mateka katika Babiloni kwa sababu ya ibada ya sanamu. (2 Wafalme 24:15). Baadaye wengine walirudi katika Yuda, japo sio wote. Hii ilitokea katika siku za Ezra na Nehemia. Wayahudi walitawanyika miongoni mwa mataifa mengine.

Wengine walibaki katika mataifa mengine (tazama Esta). Wengine walibaki katika Babiloni hata katika wakati wa Mitume. (1 Pet. 5:13… kulikuwa na kusanyiko la Bwana pale)

Kulikuwa kunakutawanyika wakati kwa wakati, lakini zilikuwa ni jamii ndogo na hazikufikia wazo la "kutawanyika kwa mataifa".

Wa tatu… ambalo ndio la mwisho na Kuu

Tawanyiko ambalo ni la kutisha ilitokea siku za utawala wa Rumi. Hii ilitabiriwa na manabii pia na Mwokozi wetu katika wakati wake dunia. Angalia ishara katika Kumb.28:15-68:

- TAI… Tai ilikuwa ni ishara ya utawala wa Rumi (ustari 49)
- USO MKALI "*Taifa lenye uso mkali, ambalo haliangalii uso wa mzee, wala halipendi kijana.*" (mustari 50)
- KUHUSURU "*…Naye atakuhusuru katika malango yako…katika nchi yako yote kila upande…*" (musatari 52)
- ULAJI WA NYAMA ZA WATU*…Nawe utakula uzao wa tumbo lako mwenyewe, nyama ya wana wako…katika mazingirwa na katika mkazo utakaokazwa na adui zako.*" (mustari 53)
- "*…juu ya mchanga wake atokaye katikati ya miguu yake, na juu ya wanawe atakaowazaa; kwa kuwa atawala kwa siri kwa uhitaji wa vitu vyote; katika mazingirwa…*" (mustari 57)
- Linganisha haya na maelezo ya matukio haya na Yesu mwenyewe. (Mat. 24:1-28)
- UKATILI "*…Laana ya maangamizi…*" (mustari 15)
- UVAMIZI "*…Walioko katika Uyahudi wakimbilie milimani.*" (mistari 16-18)
- TAUNI "*Kutakuwa na maangaiko, ambayo haijawahi kutokea tokea mwanzo wa ulimwengu hata sasa, haitatokea tena.*" (mustari 21)
- ULAJI WA NYAMA ZA WATU "*…ole wao walio na watoto na wanao nyonyesha katika siku hizo.*" (mustari 19)

Pia linganisha na maandishi ya Yosefu kuhusu tukio hili. (Yosefu alikuwa ni mwana historia wa Kiyahudi aliyeandika "maangaiko ya Wayahudi" na "Vta vya Wayahudi")

- UKATILI WA WARUMI Soma vitabu vitano na sita ya "Vita vya Wayahudi"; maelezo ni ya kweli na haijakosewa.
- UVAMIZI WA YERUSALEMU Vitabu tano na sita vinaeleza uvamizi huu na Tito (mwana wa Vespasian) na wakaidi wote waliokuwapo.
- MATESO YA WAYAHUDI WALIOVAMIWA Mateso ya sehemu ya Yerusalemu pia imeelezwa kwa undani. Mateso haya hayaaminiki.
- ULAJI WA NYAMA ZA WATU Kitabu cha sita, gawanyo 4, 201-217 inaeleza ukatili huu wa ajabu, mbaya kiasi kwamba Warumi, wakiisikia, walitishwa.

Haiwezi kupingwa kwamba hivi vyote vinaelezea tukio moja. Janga hili lililengwa kwa taifa la Kiyahudi, baada ya hapo, taifa lilizingirwa na kuchukuliwa mateka katika ufalme wa Rumi yote kama watumwa. Kulingana na historian ya kidunia, wengine walitorokea mashariki katika nafasi za Asia, ingawa Biblia haiandiki hili swala. Baadhi ya Wayahudi walibaki katika nchi zao, lakini ghafla wakawa wachache walioteswa katika nchi.

Maelezo ya kuteswa kwa Wayahudi katika uthibitisho wote wa karne haiachi shauku kwamba hawa waliotawanyika mwishoni lilikuwa limekamilika; kulikuwa hakuna taifa la Wayahudi. Walitawanyika katika mataifa yote ya ulimwengu hasa kama Mungu alivyowaonya. Lilikuwa libaki hivyo milele?

Kurudi kumeahidiwa

Mungu aliahidi kwamba hatawasahau wale waliotawanyika katika mataifa yote. "*Bwana Mungu wako atakapougeza utmwa wako, naye atakuhurumia tena atarejea na kukusanya kutoka mataifa yote, huko alikokutawanyia BWANA Mungu wako.*" (Kumb. 30:3)

Swali siyo kwamba ndiyo au hapana Mungu atatunza ahadi zake, lakini lini na kwa mfumo gani ataweza kufanya hivyo.

"Katika Siku za Mwisho"

Hesea anatuambia kwamba kurejea kutakuwa katika "…siku za mwisho". (Hosea 3:5) "*Baada ya hayo wana wa Israeli wakarejea, na Daudi mfalme wao nao watamwendea BWANA na wema wake kwa kicho siku* ***za mwisho****.*

"*Lakini mimi najua ya kuwa mteteaji wangu yu hai, na ya kuwa* ***hatimaye*** *atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mungu.*" (Ayubu 19:25-26).

Kumbuka maneno ya Paulo katika Ebr. 1:1-2, "*Mungu ambaye zamani alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,* ***mwisho wa siku hizi*** *anasema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*"

Petro anaweka wakati wa nyakati za mwisho, Mdo. 2:17, "*Itakuwa* ***siku za mwisho*** *asema Mungu, nitawamwangia watu Roho yangu na wana wenu na binti zenu watatabiri na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto.*"

Kwa mukutasari:

- Mkombozi (Kristo) atasimama **siku za mwisho** katika dunia…
- Mungu alinena kupitia Kristo **siku hizi za mwisho**…
- Petro anaonyesha Pentekoste kama ni **siku za mwisho**…

Ni katika kiwango hiki wakati ambapo kitu kinacho fanana hutokea inatoonyesha wakati na njia ambayo Mungu ataleta "urejeshi" wa Waisraeli kama jinsi alivyoahidi.

Urejeshi wa Kitaifa au Mabaki?

"*…Walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu.*" (Mdo 2:5). Hapa kulikuwa na kusanyiko la Wayahudi lililo ahidiwa na Mungu; siyo katika wazo la kitaifa, bali ni kama mabaki ya watu hawa. Lakini wengine husema, "kimsingi hii ni tafsiri yako ya mkusanyiko, lakini siyo kweli."

Mdo 15:15-17, "*…maneno ya manabii yapatana na hayo, kama ilivyoandikwa, baada ya mambo haya nitarejea, nami nitaijenga tena nyumba ya Daudi iliyoanguka. Ili wanadamu* ***waliosalia*** *wamtafute Bwana, na mataifa yote ambao jina langu limetajwa kwao;*"

Hivyo tunaona kwamba maandiko yanafundisha kwamba Mungu alileta kusanyiko la Wayahudi katika Pentekoste wakati wa "siku za mwisho", ikifuatiwa baadaye na utambulisho wa Mataifa.

Hii inashuhudiwa na Paulo katika Efe. 2:14-16, "*…yeye ndiye amani yetu aliyetufanya sisi sote tuliyokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuondoa ule uadui kwa mwili wake, ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani.*

Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba."

Siku arobaini kabla ya Pentekoste, mitume walimuuliza, "*Bwana wakati huu ndio unawarudishia Waisraeli ufalme wao?*" Bila kujali yote ambayo Yesu aliwafundisha kwa miaka mitatu, bado wanatarajia Mungu kurejesha ufalme wa kitaifa kwa Israeli.

Alfu Yesu akajibu, "*Siyo juu yenu kujua wakati au sababu, ambayo Baba ameweka katika uwezo wake.*" Hataivyo, aliwaonyesha kwamba ilikuwa imeadhimu. "*Alipokusanyika pamoja nao, akawaagiza kwamba wasitoke Yerusalemu, bali* ***wasubirie ahadi ya Baba****, ambayo ninyi mmezisikia habari zake.*" (Mdo 1:4-5 Akaonyesha kwamba hii haitakuwa "*…siku nyingi toka sasa…*" (Mustari 5)

"*Lakini mtapokea uwezo, baada ya Roho Mtakatifu kuwajilieni nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Samaria, na katika ulimwengu wote.*" (mustari 8).

Hema Ya Mungu

Mungu aliahidi kwamba "*…atajenga nyumba ya Daudi…*" (Mdo. 2:5) Nyumba ilikuwa ni hema ambalo Wayahudi walikuwa wanaabudia wakati wakiwa safarini.

Paulo akaonyesha kwamba ibada ya Mkristo inapaswa kutendeka katika hema iliyokamilika."*Lakini Kristo akiisha kuja aliye kuhani wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilify zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake isiyo ya ulimwengu huu,*" (Ebr. 9:11). Hema hii "*haikufanywa kwa mikono*". Mungu alisema, "***nitajenga*** *tena hema ya Daudi…*"

Kurudi huku kwa Israeli hakukuwa wa kitaifa chini ya agano la kitaifa la zamani la Israeli, kwa sababu chini ya agano hilo Mungu angeweza tu kuabudiwa Yerusalemu.

Kwa mama Msamaria Yesu alieleza mfumo wa ibada kuja katika kusanyiko. Mwanamke akamwambia, "*Baba zetu waliabudu katika mlima huu (Gerazini); na wewe unasema kwamba Yerusalemu ndiyo sehemu itupasapo kuabudia. Yesu akamwambia, mama unisadiki, saa inakuja ambapo* ***hamtamwabudu Baba katika mlima huu, ama Yerusalemu****. Lakini saa inakuja nayo sasa ipo ambapo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na kweli: maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu.*"

Vipi kuhusu Israeli Leo?

Nakumbuka niliposoma katika jarida letu la dini 1948, ndugu aliandika kwamba tulikuwa tunatazamia wakati wa kutimiza ahadi ya Mungu kuwakusanya Israeli warudi katika nchi yao. Hakuna chochote kinachoweza kuwa mbali na ukweli.

Kama tulivyoona, ahadi ya Mungu haikuwa katika hali ya kitaifa. Taifa la sasa la Israeli haijengwi katika mfumo wa kidini. Ni taifa la kidunia, hailindwi na maandishi ya kidini. Wayahudi wa Kiothodox ya Israeli toka kuzaliwa kwake wamekuwa wakilaumu kwamba taifa halifuati mafundisho ya sheria, na kukisia kwamba limeshaanguka.

Nyumba ya Daudi (hema) haija jengwa, hata kama baadhi wanadai kwamba itajengwa hivi karibuni. ("mwinjilisti" mmoja alitabiri kwamba hekalu litajengwa mwanzo wa 21 Milinia, 2000; haijawahi kutokea, na haitatokea).

Kuna mengi zaidi ambayo yanaweza kutazamwa kunyesha kusudi halisi ya Mungu, lakini hii inatosha kuonyesha hitimisho la kweli la kusanyiko kuwa katika Pentekoste.

Kwa upendo wa kweli,

J D Logan